# TANGAZO LA KAZI

## HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI KWA MKATABA KWA WASAIDIZI WA HESABU KATIKA VITUO VYA AFYA VYA MANISPAA YA LINDI

Mkurugenzi wa Manispaa ya Lindi anawatangazia nafasi mbili (2) ya kazi ya Mkataba ya Wahasibu wasaidizi katika Vituo vya Afya vya Manispaa ya Lindi.

**VIGEZO**

- Awe Raia wa Tanzania aliyehitimu na kupata Cheti cha Taaluma cha Kidato cha Nne (IV) (Results Slip hazikubaliki).
- Awe na **Stashahada ya Uhasibu** kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali au **Cheti cha ATEC I** kinachotolewa na **NBAA** au sifa nyingine zinazolingana na hizo zinazotambulika na **NBAA**
- Awe na umri wa miaka isiopungua 18 na usiozidi 45
- Watumishi waliofukuzwa kazi serikalini hawaruhusiwi kuomba
- Barua za maombi ziambatanishwe na nakala za vyeti vilivyothibitishwa, maelezo binafsi ya mwombaji na picha ndogo za rangi mbili(2) zilizopigwa siku za karibuni.

**KAZI NA MAJUKUMU**

- Kusimamia utunzaji wa nyaraka za fedha kwenye Vituo vya kutolea Huduma za Afya
- Kufanya usuluhishi wa kibenki kwenye Vituo vya kutolea Huduma za Afya
- Kusimamia matumizi ya fedha Vituoni kulingana na mwongozo wa matumizi ya fedha za Vituo vya kutolea Huduma za Afya na kanuni za Fedha za Serikali
- Kutoa taarifa za fedha za mapato na matumizi kila mwezi.

Maombi yote yatumwe Ofisi ya **Mkurugenzi wa Manispaa ya Lindi ,SLP 1070, Lindi** kabla ya tarehe **20/11/2020**

**Imetolewa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa Lindi.**